

# Uchunguzi wa Maana za Vipera vya Semi katika Fasihi Simulizi ya Kirundi

<sup>1</sup>Havyarimana Enoch and <sup>2</sup>Kamaro Consolée

<sup>1</sup>University of Burundi, Burundi, E-mail : [enochelle1@gmail.com](mailto:enochelle1@gmail.com)

Phone: +257 66 500 213

<sup>2</sup>University of Dar es Salaam, Tanzania

E-mail : [kamaroconsolee73@gmail.com](mailto:kamaroconsolee73@gmail.com)

Phone : +257 79 571 914

**Absract:** Oral literature is an event linked to a community way of life. In fact, political, economic, social and cultural changes cause various branches of oral literature to have specific meanings, this is according to Samwel (2020). In addition, the culture of a community affects the use of language and helps interpret oral literary works. This study therefore aimed to examine the oral literature of Burundian society by highlighting the meanings of the Kirundi expressions. This study which was conducted in Burundi, its data were collected from 15 respondents who are teachers of Kiswahili at universities located in the city of Bujumbura. The interview method was used where each respondent was given a piece of paper and asked to explain the meaning of each expression in Kirundi oral literature using at least 2 examples. Moreover, this study was guided by the Politeness Theory which was founded by Levinson (1983). The findings showed that Kirundi phraseological expressions have their meanings according to the Burundian society's way of life. The expressions of Kirundi oral literature discussed in this research paper are such as: proverbs, sayings, riddles, idioms, puns, nicknames and name riddles. This study concludes by recommending a detailed study on the status of oral literature in Burundi because it was found that some of the words of Kirundi language tend to be outdated.

**Keywords:** Burundi, oral literature, idioms, culture, society

---

## Ikisiri

Fasihi simulizi ni tukio linalofungamana na mfumo wa maisha ya jamii. Kiuhalisia, mabadiliko ya kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiutamaduni husababisha tanzu mbalimbali za fasihi simulizi kubadilika Samwel (2020). Aidha, utamaduni wa jamii huathiri matumizi ya lugha na ndio husaidia kutoa tafsiri ya kazi za fasihi simulizi. Hivyo, utafiti huu ulilenga kuchunguza fasihi simulizi ya jamii ya Warundi kwa kuangazia maana za vipera vya semi za Kirundi. Utafiti huu ambao ulifanyika Burundi, data zake zilikusanywa kutoka kwa watafitiwa 15 ambao ni walimu wa Kiswahili vyuo vikuu vinavyopatikana jijini Bujumbura. Mbinu ya usaili ilitumika ambapo kila mtafitiwa alipewa karatasi na kuombwa kueleza maana ya kila kipera cha semi katika fasihi simulizi ya Warundi kwa kutumia mifano angalau 2. Aidha, utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Upole ambayo iliasisiwa na Levinson (1983). Taarifa zilionyeshwa kuwa vipera vya semi za Kirundi vina maana zake kulingana na mfumo wa maisha wa Warundi. Vipera vya semi za fasihi simulizi ya Kirundi vilivyoadiliwa ni kama vile: methali, misemo, vitendawili, nahau, vitanzandimi, vichezeshamaneno, mafumbo, lakabu, mafumbo jina, na chemshabongo. Utafiti huu unahitimisha kwa kupendekeza utafiti wa kina kuhusu hali ya fasihi simulizi nchini Burundi kwa sababu ilibainika kuwa baadhi ya vipera vya semi za Kirundi vinaelekea kusahaulika.

**Maneno ya msingi:** Burundi, fasihi simulizi, vipera vya semi, utamaduni, jamii

---

## 1. Utangulizi

Fasihi simulizi imebeba dhana kuu mbili ambazo ni “fasihi” na “kusimulia”. Kwa kuanza, dhana ya “fasihi” inarejelea sanaa ambayo hutumia kwa ubunifu kuwasilisha masuala kuhusu maisha ya binadamu na mazingira anamoishi (Matei, 2010). Aidha, fasihi kama sanaa ya lugha imegawanyika katika makundi mawili ambayo ni “fasihi andishi” na “fasihi simulizi”. Fasihi andishi inarejelea kazi ambazo zinaandaliwa na kufikishwa kwa hadhira kwa kupitia njia ya maandishi kama vile riwaya na michezo ya kuigiza iliyoandikwa ilhali fasihi simulizi inahusu aina ya fasihi inayotolewa kwa njia ya mdomo. Kwa mujibu wa Matei (2010:5), fasihi simulizi hubuniwa na kuhifadhiwa akilini. Anaendelea kudai kuwa fasihi simulizi huwasilishwa na kusambazwa kwa masimulizi, mazungumzo ya kisanaa, kuimba, kughani, kuigiza na kukariri kwa hadhira hai. Naye Mulokozi (2017) anadai kuwa fasihi simulizi ni dhana inayotumika kuelezea fasihi itolewayo kwa mdomo bila kuandikwa. BAKITA (2017) inafasili kuwa fasihi simulizi ni aina ya fasihi inayotolewa kwa njia ya matamshi kama vile hadithi, ngonjera, vitendawili na huhifadhiwa na kurithishwa kutoka kizazi kimoja kwenda kingine kwa njia ya mdomo.

Kwa ujumla, fasihi simulizi ni sanaa inayotungwa au kubuniwa kichwani na kuwasilishwa kwa hadhira kwa njia ya mdomo na vitendo bila kutumia maandishi; yaani, katika hali ya kuimba, kusimulia, kuigiza, kughani, na kutamba. Aidha, fasihi simulizi ni tukio linalofungamana na muktadha fulani wa kijamii. Muktadha huo ni kama eneo, wakati, mazingira, na mada. Vilevile, muktadha ndio unaoamua sanaa ya fasihi simulizi ichukue umbile gani (Mulokozi: 1989). Fasihi simulizi huhifadhiwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine kwa njia ya masimulizi na kukumbukwa kama historia ya jamii mwaka baada ya mwingine. Kila msimuliaji wa kazi ya kifasihi hupewa sifa za kuwa msanii na ana uhuru wa kueleza tungo kwa umbaji wake mwenyewe.

Wanazuoni wanakubaliana kuwa fasihi simulizi inahusiana sana na jamii. Hii ina maana kuwa fasihi haitoki katika ombwe tupu bali hutokana na mifumo ya kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiutamaduni katika jamii husika (Samwel, 2020). Na ukweli ni kwamba duniani kuna jamii nyingi. Miongoni mwa jamii hizo, kuna jamii ya Warundi ambao ni wenyeji wa taifa la Burundi. Hii inamaanisha kuwa fasihi simulizi ina mashiko nchini humo. Aidha, kila jamii ina mfumo wake wa maisha na shughuli maalumu zinazoitambulisha. Mataifa mengi kama vile: Tanzania, Kenya, Uganda, Somalia, Nigeria na Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kongo huwa na makabila ambayo hufanya mataifa hayo kuwa na aina mbalimbali za utamaduni, kwa sababu kila kabila huakisi utamaduni wake. Samwel (2020) anadai kuwa utamaduni wa jamii ndio husaidia kutoa tafsiri ya kazi ya fasihi simulizi. Anaongeza kuwa utamaduni wa jamii huathiri matumizi ya lugha katika tanzu za fasihi simulizi za jamii husika. Hii ina maana kuwa uteuzi wa maneno katika tanzu za fasihi simulizi utatokana na utamaduni wa jamii hiyo.

Tofauti na mataifa mengine, taifa la Burundi halina makabila yanayotofautiana kiutamaduni na kilugha; yaani, nchi nzima ina wakazi ambao wanazungumza lugha mama moja. Kwa mujibu wa BAKITA (2017), kabila ni jamii ya watu wenye lugha, mila na desturi na mfumo mmoja wa maisha. Na mfumo huo ndiyo hubeba fasihi ya jamii hiyo. Kwa mantiki hiyo, hatuna budi kukazia kwamba fasihi, iwe andishi ama simulizi, inapatikana kulingana na utamaduni (mfumo wa maisha) wa jamii au kabila husika. Pamoja na juhudi za watafiti za kuainisha tanzu za fasihi simulizi bado kuna utata wa kuelezea fasihi simulizi ya Warundi hasa utanzu wa semi na dhima yake. Hali hii inaelezwa na uhaba wa tafiti katika uwanja wa fasihi simulizi. Pia, walimu nchini Burundi hutumia kwa kiwango kikubwa vitabu vya kifaransa kufundisha fasihi simulizi. Kwa kawaida, kuna uhaba mkubwa wa tafiti katika taaluma za Kiswahili nchini humo (KAKAMA 2019). Uhaba wa tafiti ndio ulituacha na maswali kadhaa ya kujiuliza kuhusu fasihi simulizi hasa kwa kuzingatia utanzu wa semi: je, vipera vya Semi katika fasihi simulizi ya Warundi vina maana gani? Hivyo, utafiti huu ulilinga kuchunguza fasihi simulizi ya Kirundi kwa kuweka mkazo kwenye maana za vipera vya semi.

### 3. Nadharia ya utafiti

Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Upole ambayo iliasisiwa na Levinson (1983). Nadharia hii inasisitiza umuhimu wa muktadha katika kutoa maana ya maneno na uelewa wa vitamkwa katika mawasiliano. Kulingana na Levinson, maana haitokani na maneno au misemo ya mtu binafsi pekee bali inaundwa na vipengele vya kimuktadha na maarifa na dhana zinazotumika kati ya wazungumzaji.

Levinson anaangazia kanuni ya muktadha, ambayo inarejelea wazo kwamba wazungumzaji hutumia viashiria vya muktadha kufasiri maana ya maneno na vitamkwa kwa usahihi. Vidokezo hivi vya muktadha ni pamoja na vipengele kama vile mazingira ya kimwili, mazungumzo ya awali, ujuzi wa washiriki, na kanuni za kitamaduni. Maoni yake yanashabihiana na yale ya Horn (1990) anayedai kuwa maneno yanaweza kuungana na kuwasilisha maana tofauti na maana za maneno teule yaliyotumiwa pamoja kutegemea mazingira ambamo maneno hayo yanatumiwa. Uelewa wa wanajamii wa kanuni za msingi zinazotawala matumizi ya lugha ndio utasababisha maelewano kati yao wakati kazi ya fasihi inayoshughulikiwa inawasilishwa miongoni mwao. Levinson anasema kuwa muktadha, unaojumuishia hali, uhusiano, na vipengele vya kitamaduni vya mawasiliano, ni muhimu katika kutatua utata unaoeweza kutokea au tafsiri nyingi zinazowezekeka za matamshi. Bila muktadha unaofaa, maana kamili iliyokusudiwa inaweza isieleweke kwa usahihi.

Yule (1996) anasema kuwa muktadha ni mazingira ya ulimwengu ambapo neno linatumika. Kwa upande wake, Widdowson (1996) anaeleza muktadha kama vipengele vya hali vinavyotawala matumizi halisi ya lugha vinavyochukuliwa kuwa faafu kwa maana iliyokusudiwa. Anaongeza kuwa muktadha ni kijenzi cha kiakili. Kwa mujibu wa Yule (1996), kazi yoyote ile ya fasihi ina muktadha wa kijamii. Lugha ya fasihi hutumiwa kitamathali. Katika lugha hii, kuna matumizi ya sitiari, jazanda, taashira na kaida nyingine za lugha. Maana zilizokusudiwa katika kazi hizo za kisanii hufumbwa na fanani au mwandishi na hivyo basi huhitaji hadhira au wasomaji kufumbua maana hizo.

Kwa hivyo, kulingana na Levinson, kuelewa maana inayokusudiwa na mzungumzaji hutegemea sana kuzingatia muktadha wa mawasiliano, ikijumuisha maarifa ya pamoja, mawazo, na kanuni za kijamii zinazounda ufasiri na uelewa wa kipragmatiki wa maneno na matamshi. Muktadha hutoa viashiria muhimu vya muktadha ambavyo husaidia kufasiri na kutofautisha maana ya maneno na vitamkwa katika mawasiliano.

Nadharia ya Upole ya Levinson, ingawa ililenga hasa mikakati ya upole katika mawasiliano, bado inaweza kutoa umaizi muhimu na kuongoza utafiti juu ya uchanganuzi wa utanzu wa semi za Kirundi na dhima yake katika miingiliano ya kijamii. Nadharia hii ilifaa kuongoza utafiti huu kwa sababu zifuatazo:

Kwanza, Nadharia ya Upole inazingatia uchanganuzi wa muktadha ili kuelewa lugha tamathali. Msisitizo wa Levinson juu ya umuhimu wa muktadha unalingana na uchunguzi wa vipera vya semi za Kirundi. Kuchunguza vipengele vya muktadha vinavyoathiri matumizi na tafsiri ya tanzu za semi nchini Burundi kunaweza kutoa uelewa wa kina wa aina za semi za Kirundi na dhima yake. Hii ni pamoja na kuzingatia kanuni za kitamaduni, mahusiano ya kijamii na hali ambayo huathiri njia ambazo semi za Kirundi hutumiwa.

Pili, nadharia hii inasisitiza maarifa ya kipragmatiki ili kuelewa semi za Kirundi. Nadharia ya Levinson inaweza kuongoza uchanganuzi wa semi na namna zinavyobeba maana ya ziada iliyodokezwa au isiyo ya moja kwa moja zaidi ya tafsiri halisi. Kuchunguza jumbe zinazodokezwa, athari za kipragmatiki, na matumizi ya mbalimbali ya semi katika muktadha wa Burundi kunaweza kutoa mwanga juu ya maana zake katika mawasiliano na mwingiliano wa kijamii.

Mwisho, Nadharia ya Uople inazingatia utamaduni wa jamii. Utambuzi wa Levinson wa athari za vijenzi vya utamaduni wa jamii juu ya mwenendo unaokubalika katika mawasiliano unaendana na kuchunguza vipera vya semi za Kirundi. Kuelewa jinsi semi za maneno zinavyoakisi maadili ya kitamaduni, imani na kanuni za kijamii kunaweza kutoa maarifa kuhusu utambulisho wa kitamaduni, nguvu na urithi wa lugha ya jamii ya Burundi.

Kwa kuunganisha maarifa ya Nadharia ya Upole ya Levinson, utafiti huu ulichunguza maana za vipera vya semi katika fasihi simulizi ya Warundi.

#### 4. Mbinu za utafiti

Lengo mahususi la utafiti huu lilikuwa kuchunguza maana za vipera vya semi katika fasihi simulizi ya Warundi. Uchunguzi ulifanyika katika vyuo vikuu vilivyopo katika jiji la Bujumbura nchini Burundi. Sampuli ya watoataarifa ilikuwa ni walimu wa Kiswahili 15 waliogawika katika jinsia mbili: wanawake 3 ambao ni sawa na asilimia 20, na wanaume 12 ambao ni sawa na asilimia 80. Usampulishaji ulizingatia uzoefu angalau wa miaka mitano wa kufundisha Kiswahili ili mtafiti apata watoataarifa wanaofaa kwa utafiti wake. Mbinu mbili za kukusanya data zilitumika katika utafiti huu. Kwanza mtafiti alitumia hojaji. Mbinu hii ililenga kupata taarifa binafsi za watoataarifa kama vile jinsia, umri, kiwango cha elimu na uzoefu wa kazi. Pili, mbinu ya usaili ilitumika ambapo kila mtoataarifa alipewa karatasi na kujieleza kuhusu suala ifuatayo:

*Kwa kutumia mifano angalau 2, eleza maana ya kila kipera cha semi katika fasihi simulizi ya Warundi.*

Kuhusu uchanganuzi wa taarifa, utafiti huu ulitumia uchanganuzi wa data unaendana na mkabala wa kimaelezo ulioasisiwa na Miles na Huberman (1984) uitwao Jedwali “*Conceptually clustered matrix*”. Wataalamu hao wanasisitiza utumiaji wa jedwali la dhana mfanano, kwa sababu humrahisishia mtafiti kuandika uchanganuzi wake kiurahisi. Mtafiti alizikusanya data, alizichuja, na kuzitia nambari na baadaye alizifanya sentensi kamili ili ziweze kuandikika.

#### 5. Matokeo ya utafiti

Sehemu hii inachambua na inajadili matokeo ya utafiti uliofanyika katika vyuo vikuu, Chuo Kikuu cha Burundi na Chuo cha Walimu, vilivyopo jijini Bujumbura, kuhusu uchunguzi wa maana za vipera vya semi za fasihi simulizi ya Kirundi. Uchambuzi wa taarifa zilizokusanywa kwa watafitiwa 15 ulibaini tanzu za semi nchini Burundi kama ifuatavyo:

##### 1. Methali

Kuhusu kipera cha methali, watafitiwa 15, sawa na asilimia 100, walieleza kwamba methali ni kipengele muhimu cha semi katika fasihi simulizi ya Warundi. Pia, ni usemi mfupi wa kimapokeo. Methali husisimua na kuwasilisha fikra au mafunzo mazito yaliyotokana na tajriba; yaani, uzoefu wa jamii husika. Istilahi “methali” inatokana na neno la kiarabu lenye maana ya “mfano”. Hivyo, methali ni kauli inayofundisha kwa mifano au ufananisho (umithilisho) au uelekezi (kielelezo). Kwa kawaida, methali ni tungo fupi za sentensi moja ambazo hutoa funzo fulani kwa njia ya mafumbo. Methali huwa na sehemu mbili. Sehemu ya kwanza hutoa hoja, sehemu ya pili nayo hutoa suluhisho.

Taarifa zilionesha kwamba Warundi wana tabia ya kutumia sana methali haswa katika uhutubiaji. Ni vigumu kupata hotuba ambayo haina methali ndani yake.

Hii ni baadhi ya mifano ya methali iliyotolewa:

- Uwitonze/ amira ibinoze: *Mwendapole hajikwai.*
- Bukebuke/ ni rwo rugendo: *Polepole ndo mwendo*
- Isorosoro igwirira iyo iroye: *Haba na haba hujaza kibaba*
- Igiti kigororwa/ kikiri gito: *Samaki mkunje angali mbichi.*

- Ukwiga ntibihera: *Elimu haina mwisho*
- Intango igira iherezo: *Lenye mwanzo lina mwisho*
- Amaso ntiyimirwa: *Macho hayana mipaka*

## 2. Misemo

Kwa upande wa misemo, watafitiwa 13 sawa na asilimia 86,6 walidai kuwa misemo ni neno linaloibuka katika lugha ya wanajamii na kutumiwa na watu kadhaa kisha huweza kupotea au kubaki katika msamiati rasmi wa lugha ya wanajamii hao. Aidha, misemo ni semi za muda na mahali maalumu ambazo huzuka na kutoweka kulingana na muda au mazingira maalumu. Watafitiwa hao waliendelea kueleza kwamba misemo ikipata mashiko ya kutosha katika jamii huweza kuingia katika kundi la methali, vitendawili vya jamii husika. Mbali na hayo, misemo ni kauli za kejeli, za kuficha upinzani, uhasama kwa jambo linalohusika, na ni kipimo cha urazini na mkabala wa wanajamii kujihusisha na jambo hilo.

Mifano kadhaa ya misemo ilitolewa:

- Dukora dusenga, dusenga dukora  
*Tufanye kazi tukiomba, tuombe tukifanya kazi.* (Tafsiri yetu)
- Caratuvunye  
*Nchi ilituhangaisha.* (Tafsiri yetu)
- Leta mvyeyi  
*Serikali mzazi.* (Tafsiri yetu)
- 1972 twarumvise, 1993 twarabonye, 2015 twaratahuye  
*1972 tulisikia, 1993 tuliona, 2015 tulielewa.* (Tafsiri yetu)

## 3. Nahau

Watafitiwa 15 sawa na asilimia 100 walielezea nahau kama usemi mfupi unaotumia maneno ya kawaida, lakini yakiwa na maana iliyojificha na iliyotofauti na maana ya kawaida. Ni aina ya misemo ambayo imepata mashiko katika jamii fulani na kuwa sehemu ya lugha baada ya kusanifishwa. Kama ilivyo kwa lugha zingine, lugha ya Kirundi inatumia nahau kwa kiasi kikubwa

Hii ni baadhi ya mifano ya nahau iliyotolewa na watafitiwa:

- kugira umunwa muremure  
*Kuwa na mdomo mrefu* (Tafsiri yetu)  
Ina maana ya kuwa mtu asiyetunza siri.
- Kugwa bukumbi  
*Kufariki ghafla* (Tafsiri yetu)  
Ina maana ya kupoteza maisha ghafla.
- Kuragirira inaruma  
*Kuchungia mifugo mjomba wako* (Tafsiri yetu)  
Ina maana ya kufanyia kazi mtu akakunyima mshahara
- Guca urwananiye Ngoma  
*Kuamua kesi iliyomshinda Ngoma* (Tafsiri yetu)  
Ina maana ya kuamua kesi hatari zaidi inayoweza kukusababishia kifo
- Gutubika umukanda  
*Kufunga mkanda* (Tafsiri yetu)  
Ina maana ya kuwa katika hali mbaya ya kukosa chakula
- Kubura ayo ucira nay'umira  
*Kukosa ya kutema na kumeza* (Tafsiri yetu)  
Ina maana ya kukosa njia ya kujitoka katika hali tatanishi
- Kugendera mu makanda  
*Kufuata nyayo* (Tafsiri yetu)  
Ina maana ya kuiga tabia ama kufuata mawazo ya mwingine

## 4. Vitanzandimi

Watafitiwa 8 sawa na asilimia 53, 3 walifasili vitanzandimi kuwa ni kauli zenye maneno yenye mchanganyiko au mfuatano wa sauti zinazotatanisha kuzitamka. Kauli hizi husaidia kukuza msamiati na kuwazoeza watoto matamshi ya maneno wanapokuwa wakijifunza lugha. Aidha, watafitiwa hao hawakutofautiana kusema kwamba vitanzandimi ni sawasawa na vitate. Waliongeza kuwa vitanzandimi vinatumika katika fasihi simulizi ya jamii ya Warundi na kuwa ni maneno ambayo mara nyingi hutumiwa na watu wa rika moja, haswa vijana.

Mifano kadhaa ilitolewa na watafitiwa:

• Babwire babwirane ko bababwiye babwire abavyeyi babo ko ejo bazobabwira umwimbu w'ubwira bwabo  
*Waambie waambizane kwamba wamewaambia wawaambie wazazi wao kwamba kesho wataambiwa kuhusu mavuno ya jasho lao.* (Tafsiri yetu)

- Bareke barya bahagarikizi babiri barye umuceri wabo  
*Waache wale wasimamizi wawili wale wali wao.* (Tafsiri yetu)
- Yamugambaniye nyakugamba amagambo atagambika ku Bagamba b'I Mugamba!  
*Amemsaliti angeongea maneno yasiyoongeleka kwa Wagamba kutoka Mugamba!* (Tafsiri yetu)

#### 5. Vichezsha maneno

Watafitiwa 14 sawa na asilimia 93, 3 walikubaliana kuwa vichezsha maneno ni miongoni mwa semi zinazopatikana katika jamii ya Warundi lakini zinazoelekea kupotea. Kauli hizi ni semi zenye kucheza maneno au sauti zinazofanana. Kwa kawaida, kauli hizi hutumiwa na watu wenye uhusiano wa karibu sana na wanaotaka kuficha mambo yao. Aidha, vichezsha maneno huchukuliwa kama lugha ya wahuni na ni ngumu kuandika ama kubaini kuinachoongelewa kwa mtu ambaye hayumo kwenye kundi la wazungumzaji hao.

Hii ni baadhi ya mifano iliyotolewa :

- Isingoso tusugesendese gusukisinasa tusurasagasarusukasa hasanyusumasa  
*Njooni twende kucheza tutarudi baadaye*
- Asabasanasa basarasakosomeseyese ?  
*Watoto wazima ?*
- Asabasanyeseshuresese bososese basazosogasarusukasa esejoso  
*Wanafunzi wote watarudi kesho*
- Asabasavyeseyisi basajese gusutosorasa asabasanasa basaboso  
*Wazazi wamekuja kuchukua watoto wao*

#### 6. Vitendawili

Watafitiwa 12 sawa na asilimia 80 walijadili kwamba vitendawili ni usemi wenye mafumbo. Vitendawili ni fungu la maneno la kimapokeo ambalo hufumbwa na mtu mmoja kwa madhumuni ya kuzua mambo mbalimbali kuhusiana na masuala tofauti katika maisha na mazingira ya jamii. Fungu hilo hushirikisha pande mbili: anayetega na anayetegua. Aidha, kitendawili ni swali ambalo huulizwa kwa hadhira ili lipate ufumbuzi. Swali hilo huwa linafahamika kwa jamii hiyo na kwa washiriki katika mazungumzo hayo. Taarifa za watafitiwa zilionyeshwa kwamba vitendawili vipo katika fasihi simulizi ya Warundi lakini vinaelekea kusahaulika kutokana na maendeleo ya utandawazi.

Hii ni mifano kadhaa ya vitendawili vya Warundi:

- Sokwe! Niruze. Sokwe! Niruze. Ndaye hejuru ndanungwa! = umuhwi  
*Kitendawili! Tega! Kitendawili! Tega! Nimeangalia juu nikapatwa na hamu! = ndizi mbivu* (Tafsiri yetu)
- Sokwe! Niruze. Sokwe! Niruze! Akana kanje ko kuneshwa mutangana! = uruyuki  
*Kitendawili! Tega! Kitendawili! Tega! Mtoto wangu anaweza kukushinda japo hamlingani! = nyuki* (Tafsiri yetu)
- Sokwe! Niruze. Sokwe! Niruze! Ndakibona sindagifata = Igitutu  
*Kitendawili! Tega! Kitendawili! Tega! Ninakiona hakishikiki =Kivuli* (Tafsiri yetu)
- Sokwe! Niruze. Sokwe Niruze! Nkubise aho hepfo ndanezerwa: Ikigori  
*Kitendawili! Tega! Kitendawili! Tega! Ninaenda hapo chini nikafurahi: Mhindi* (Tafsiri yetu)

#### 7. Chemshabongo

Kipera kingine cha semi za Kirundi kilichojadiliwa ni chemshabongo. Kuhusu kipera hiki, watafitiwa 9 sawa na asilimia 60 walidai kuwa Chemshabongo ni maswali ambayo humtaka mtu kutumia akili na ujuzi kuyajibu. Maswali mengi ya aina hii ni ya kimapokeo, mengine hubuniwa na msemaji ili kukidhi mahitaji ya hadhira mahususi. Baadhi ya chemshabongo, kwa hakika, ni hesabu tu. Nyingine hutolewa kwa njia ya mraba ambao unahitaji kujazwa kwa maneno mwafaka. Pamoja na kumhitaji mtu kutumia uhalisia wa mambo, anahitajika kutumia mantiki ili kujibu maswali ya aina hiyo.

Mifano iliyotolewa:

- Hagati y'ikiro c'ipampa n'ikiro c'amabuye ni ikihe kiremereye?  
*Kati ya kilo moja ya pamba na kilo moja ya mawe kipi kizito?* (Tafsiri yetu)
- Inyuma y'urupangu rwa mbere rwa Yohani hari urupangu, kandi imbere y'urupangu rwiwe rwa mbere hari urundi. None Yohani afise impangu zingahé?  
*Nyuma ya jengo la kwanza la Yohana kuna jengo, vilevile mbele ya jengo lake la kwanza kuna jengo jingine. Je, Yohana ana majengo mangapi?* (Tafsiri yetu)

#### 8. Lakabu

Watafitiwa walijadili pia kuhusu lakabu, kimojawapo mwa vipera vya semi. Asilimia 73, 3 za watafitiwa zilionesha kwamba lakabu ni jina la msimbo au jina la kupanga ambalo mtu hujibandika ama hubandikwa kutokana na sifa zake za kimaumbile, kitabaka, kitabia au kimatendo. Lakabu aghalabu huwa neno moja au fungu la maneno lililo na maana fiche au ya kisitiari.

Baadhi ya mifano iliyotolewa kuhusu lakabu ni hii ifuatayo :

- Kirogorogo: Anayesema mengi bila kuficha
- Rutwe : Ana kichwa kikubwa
- Sebarundi: Mfalme
- Inababiri : Mwanamke aliyeeza mapacha
- Mamaburundi: Mke wa rais wa Burundi

## 9. Mafumbo jina

Kipera cha mafumbo jina kilijadiliwa katika utafiti huu. Watafitiwa 10 sawa na asilimia 66, 6 walieleza kwamba mafumbo jina yanahusu majina yote ya ukoo yanayopewa watoto siku ya kuzaliwa. Majina kama Kezakimana, Munezero, Iteka, na kadhalika, hurejelewa kama mafumbo jina kwa sababu wazazi wa mtoto huwa na maana yao kumuita mtoto hivyo. Mafumbo jina yanatofautiana na lakabu. Utofauti ni kwamba lakabu ni jina la kupanga (iritazirano kwa Kirundi) na ambalo mtu huweza kupewa wakati wowote wa maisha yake kutokana na sababu fulani ilhali fumbo jina ni jina la ukoo ambalo mtu hupeva siku ya kuzaliwa na ni jina ambalo linatambulika kwa serikali. Pia, watafitiwa hao walijadili kwamba mafumbo jina ya Warundi huhusisha Mungu kwa kiasi kikubwa.

Hii ni baadhi ya mifano ya mafumbo jina:

- Nizigiyimana : Ninatumaini Mungu
- Ndikumana : Nipo kwa Mungu
- Nduwimana : Mimi ni wa Mungu
- Havyarimana : Mungu ndiye anazaa
- Mucowimana : Nuru ya Mungu
- Nshimirimana : Ninamshukuru Mungu

## 10. Mafumbo

Kuhusu usemi wa mafumbo, taarifa zilibaini kuwa mafumbo yapo kwenye fasihi simulizi ya Kirundi na ni aina ya semi zinazotumiwa sana na Warundi katika kuwasiliana. watafitiwa 12 sawa na asilimia 80 walidai kuwa mafumbo ni kauli zenye maana iliyojificha. Mafumbo hutumia lugha fiche au ya kiistiari pamoja na tamathali nyingine za usemi. Aina hii ya usemi humtaka anayambiwa kudadisi mazingira yake na kufikiria ili kupata maana. Mafumbo huchemsha bongo za wale wanaoshiriki katika kuyafumbua. Watafitiwa waliongeza kuwa mafumbo kwa kawaida ni semi za aina ya vitendawili lakini ndefu. Aidha, mafumbo hutumika sana sana katika mazungumzo au huundwa kutegemea mazingira. Kauli za mafumbo za aina hii ni kama vile *Imigani ya Samandari* (vitendawili vya Samandari), *Imigani ya Inarunyonga* (vitendawili vya Inarunyonga) n' *Utujajuro* (kauli za kuchekesha).

Hii ni baadhi ya mifano ya mafumbo iliyotolewa :

- Babajije Samandari bati : "Urabona ga Samandari ngo wenda umupfu ?" Nawe ati: "Yapfuye yari yarakinyemereye." *Walimuuliza Samandari : " Kwa nini unafanya tendo la ngono na maiti ?" Akajibu: "Alikuwa ameniahidi kabla hajafariki."* (Tafsiri yetu)
- Imbwa bayikubitiye ku mugezi irabweja iti: "Ni ivyago binguyeko nakare sinahora mvoma." *Mbwa alipigwa mtoni akabweka eti: " Ni kisanga kimenikuta; haikuwa kawaida yangu kuchota maji."* (Tafsiri yetu)

## 6. Hitimisho

Maana za vipera vya semi zinaonekana kujadiliwa kwa mitazamo tofautitofauti. Hilo lilidhihirika pia katika kueleza vipera vya semi za Kirundi. Wapo watafitiwa waliodai kuwa vipera kama vile lakabu na mafumbo jina hujumuishwa katika kipera kimoja, vivyo hivyo kwa vitendawili, chemshabongo na mafumbo. Fasihi simulizi siyo taaluma tuli, inabadilika kutokana na sababu kadhaa wa kadhaa; mabadiliko ya kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiutamaduni husababisha tanzu mbalimbali za fasihi simulizi kubadilika. Pamoja na hayo, semi za Kirundi ni muhimu sana kuzichambua na kuzijua ili kuweza kuchangamana kwa urahisi na Warundi kwa sababu mawasiliano yao yanazingatia sana matumizi ya lugha tamathali. Aina za semi kama vile: methali, vitendawili, misemo, lakabu, mafumbo jina, chemshabongo na mafumbo zilionekana kuwa muhimili na kitambulisho cha fasihi simulizi ya Warundi. Aidha, fasihi simulizi haiwezi kuchambuliwa pwekepweke bila kuzingatia mfumo wa maisha ya jamii husika. Kwa kuangalia tu majina ya Warundi ni sababu tosha kwamba fasihi simulizi ya Kirundi ni hai japokuwa kuna baadhi ya vipera vya semi vinavyoelekea kusauhauka kutokana na mabadiliko ya mfumo ya kimaisha kuelekea utandawazi. Pamoja na umuhimu wake katika jamii, kama

vile kuelimisha, kuonya, kuburudisha, kujifunza lugha, na kadhalika, vitendawili na vichezeshamaneno vinaelekea kupotea. Hivyo, utafiti huu unahitimisha kwa kupendekeza utafiti wa kina kuhusu hali ya fasihi simulizi nchini Burundi. Vilevile, tafiti za kina kuhusu ufundishaji wa fasihi simulizi nchini humo zinaweza kuwa na mchango mkubwa katika kuongeza idadi ya marejeleo na katika kubuni mikakati faafu ya kutunza fasihi hiyo.

#### **MAREJELEO**

BAKITA (2017 : Toleo la pili). *Kamusi Kuu ya Kiswahili*. Longhorn Publishers (T) Ltd. Dar es Salaam.

Choge, S.C. (2020). Uenezi wa Kiswahili baada ya Uhuru wa Afrika Mashariki kwa Mtazamo wa Nadharia ya Mifumo Changamano. Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Masinde Muliro. *Kioo cha Lugha 2020, 18: 1-21*.

KAKAMA (2019). Ripoti: Capacity Assessment of the Development and Use of Kiswahili in the EAC. Zanzibar.

MACHIRA, S. (2015). Uchambuzi wa mikakati ya upole kama inavyotumiwa na wahusika wakuu katika tamthilia ya mbaya wetu. Tasnifu ya Shahada ya Uzamili. Chuo Kikuu Cha Nairobi.

Matei, A. K. (2010). *Fani ya Fasihi Simulizi kwa Shule za Upili*. Oxford .

Menn, J.M. (2017). *Tafsiri ya Biblia*. Equipping Church Leaders- East Africa.

Mrikaria, S. E. (2007). Fasihi Simulizi na Teknolojia Mpya. *Swahili Forum 14 (2007): 197- 206*

Mulokozi, M.M. (1996). Tangu za Fasihi Simulizi. *TUKI. Dar es Salaam*.

Mulokozi, M. M. (2017). Tangu za fasihi simulizi. *Mulika.21:1-24. Dar-es-salaam*.

Samwel, M. (2020). Hali ya Fasihi Simulizi ya Kiswahili katika Jamii ya Sasa na Mustakabali wake. *Kioo cha Lugha 2020, 18: 189-207*.

WANJALA, F. S. (2015). Mwingilianotanzu katika fasihi simulizi ya kiafrika: mfano wa embalu na mwaka kogwa. Tasnifu ya Shahada ya Uzamifu. Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Yule, G. (1996). *Pragmatics*. Oxford: Oxford University Press.